CHAKITA
CHAMA CHA KISWAHILI CHA TAIFA

ISSN: 2789-9209

# TAALUMA

## Jarida la CHAKITA

Juzuu 1 Na.1

Novemba 2021

© CHAKITA

Limechapishwa 2021

Chapa ya Kwanza 2021

ISSN 2789-9209

## Bodi ya Uhariri

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Prof. John M. Kobia | Mhariri Mkuu – Chuo Kikuu cha Chuka |
| 2. | Dkt. Leonard Chacha Mwita | Mhariri Msaidizi – Chuo Kikuu cha Kenyatta |
| 3. | Prof. Mosol Kandagor | Chuo Kikuu cha Moi |
| 4. | Prof. Evans Mbuthia | Chuo Kikuu cha Nairobi |
| 5. | Dkt. Fred Wanjala Simiyu | Chuo Kikuu cha Kibabii |
| 6. | Dkt. Joseph Nyehita Maitaria | Chuo Kikuu cha Karatina |
| 7. | Dkt. Sheila P. Wandera-Simwa | Chuo Kikuu cha Laikipia |
| 8. | Mwl. Maina T. Sammy | Chuo Kikuu cha Moi |
| 9. | Prof. Pendo Malangwa | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| 10. | Dkt. Caroline Asiimwe | Chuo Kikuu cha Makerere |
| 11. | Dkt. Caren Nyandiba | Chuo Kikuu cha Rongo |
| 12. | Dkt. Mahero Toboso | Chuo Kikuu Kishirikishi cha Alupe |
| 13. | Dkt. Naomi Nzilani Musembi | Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga |

## Washauri wa Wahariri

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Prof. Inyani Simala | Chuo Kikuu cha Masinde Muliro |
| 2. | Prof. Nathan Ogechi | Chuo Kikuu cha Moi |
| 3. | Prof. Clara Momanyi | Mtaalamu wa Kiswahili-Nairobi |
| 4. | Prof. Kitula King'ei | Chuo Kikuu cha Kenyatta |
| 5. | Prof. Kimani Njogu | Twaweza Communications |
| 6. | Prof. Leonard Muaka | Rais, CHAUKIDU, Marekani |
| 7. | Prof. Clarissa Vierke | Chuo Kikuu cha Bayreuth, Ujerumani |
| 8. | Prof. Iribe Mwangi | Chuo Kikuu cha Nairobi |
| 9. | Prof. Isaac Odeo Ipara | Chuo Kikuu cha Kibabii |
| 10. | Dkt. James Ontieri | Chuo Kikuu cha Rongo |
| 11. | Prof. Sangai Mohochi | Chuo Kikuu cha Kibabii |
| 12. | Prof. Kineene wa Mutiso | Chuo Kikuu cha Nairobi |

# Yaliyomo

Lugha na Uana: Sakata ya Nafsi
*Clara Momanyi*........................................................................................1

Pambano Dhidi ya Hejemonia ya Kizungu katika Jamii za Kiafrika: Mfano wa Mhusika Lawino katika *Wimbo Wa Lawino*
*Wendo Nabea*........................................................................................9

Kiswahili na Maendeleo Mashambani nchini Kenya
*Makoti Vifu Saidi*........................................................................................19

Nafasi ya Utamaduni katika Tafsiri: Mfano wa Msamiati wa Serikali na Bunge
*Miriam Osore*........................................................................................27

Nadharia ya *Metausasa* katika Fasihi: Mifano kutoka *Shujaaz*
*Mburu C. Kiarie, Abdulrahim Taib* na *Raphael N. Gacheiya*..................................35

Sitiari katika Bembelezi za Watikuu
*Lina Akaka, Sheila Wandera-Simwa* na *James Ogola Onyango*...............................43

Maana na Maumbo ya Unyambulishaji wa Vitenzi katika Kigĩchũgũ
*Magdalene Wangu Gituru* na *John M. Kobia*..................................................53

Uchi kama Mkakati wa Kuimarisha Usalama miongoni mwa Babukusu katika Utendaji wa *Embalu*
*Fred Wanjala Simiyu*........................................................................................65

Methali za Kiswahili katika Ubainishaji na Uhifadhi wa Mazingira
*Joseph Nyehita Maitaria* na *Leonard Chacha Mwita*..........................................73

Ufupishaji kama Mkakati wa Uundaji wa Istilahi za Kiswahili zinazotumika katika Kompyuta
*Stanley Adika Kevogo, Jackline Njeri Murimi* na *James Omari Ontieri*.....................83

Matumizi ya Teknohama na Lugha ya Kiswahili kama Nyenzo ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo: Tathmini ya Majukwaa ya *Youtube* na *Facebook*
*David Kihara* na *Pamela M. Ngugi*........................................................................93

Nafasi ya Kiswahili katika Utekelezaji wa Ajenda Nne Kuu: Uzalishaji Viwandani
*Basilio Gichobi Mungania*........................................................................................101

Fasihi Andishi kama Kurunzi ya Kuangazia Uozo katika Ndoa za Kisasa
*Naomi Nzilani Musembi*........................................................................................111

# Nafasi ya Utamaduni katika Tafsiri: Mfano wa Msamiati wa Serikali na Bunge

*Miriam Osore*

**Ikisiri**

*Wataalamu wengi wanakubaliana kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya tafsiri na utamaduni. Wananadharia wa nadharia ya tafsiri wa awali akiwemo Catford walichukulia tafsiri kama utaratibu unaohusisha hali ya kuchukua makala katika lugha moja na kuyabadilisha katika lugha nyingine kwa kuhakikisha kwamba maana katika lugha mbili zinazohusika zinalingana. Maelezo kama haya yalisisitiza kwamba tafsiri ni mchakato wa kiisimu. Katika miaka ya hivi karibuni tafsiri inachukuliwa kuwa na uhusiano na utamaduni wa lugha asilia na wa lugha pokezi. Maoni haya yanaongozwa na ukweli kwamba lugha sio tu njia ya mawasiliano bali hubeba utamaduni wa watu wanaoitumia kama lugha yao ya kwanza. Ni vigumu kutenganisha lugha na utamaduni. Kwa sababu hii shughuli yoyote ya tafsiri huhusisha lugha na utamaduni. Utamaduni ni jumla ya taratibu za maisha ya jamii. Taratibu hizi ni pamoja na mila na desturi, amali, itikadi, mielekeo, falsafa na utawala. Kwa hivyo, kwa njia hii sababu ya kufanya tafsiri ni kuendeleza mawasiliano kati ya jamii au nchi tofauti tofauti. Mtaalam wa tafsiri, Eugene Nida, amefafanua tafsiri kama mchakato unaohusisha kuzalisha makala asilia katika lugha pokezi kupitia visawe vya karibu katika kiwango cha maana na cha mtindo. Anasema kwamba ili lengo hili litimie lazima mtafsiri azingatie tofauti za kitamaduni kwa sababu tafsiri sio tu mchakato unaohusu umilisi wa lugha zinazohusika bali pia wa tamaduni zinazohusika. Msimamo wa makala hii ni kwamba tafsiri ni utaratibu unaohusu mwingiliano kati ya tamaduni mbili. Ni katika muktadha huu ambapo makala hii inachunguza jinsi ambavyo utamaduni wa Waingereza ulivyokutanishwa na wa Waswahili kupitia tafsiri za msamiati wa serikali na bunge. Data itakayochanganuliwa inatokana na vyombo vya habari na tafsiri zinazofanyika katika bunge la Afrika. Lengo la uchanganuzi huu ni kubainisha mbinu zinazotumiwa katika kutafsiri msamiati wa serikali na bunge. Pia utaangazia iwapo tafsiri hizo zinahifadhi utamaduni asilia (foreignization) ama kuhifadhi utamaduni wa lugha pokezi (familiarization) au kuchanganya yote mawili. Makala itachangia katika kutoa mapendekezo ya kuimarisha tafsiri za kitamaduni kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.*

**Maneno Muhimu:** *Tafsiri, Utamaduni, Serikali, Bunge.*

### Utamaduni, Lugha na Tafsiri

Dhana ya utamaduni inaweza kufafanuliwa kama jumla ya tabia au mienendo ya jamii maalumu. Kwa mujibu wa Guo (2012) na Bryam (2008), utamaduni ni mfumo wa mila na desturi, tabia, amali, itikadi, imani na lugha ya jamii mahsusi. Naye Nida (1964) anabainisha nguzo kuu tano za utamaduni: Utamaduni wa kidini, utamaduni wa kimazingira, utamaduni wa vifaa, utamaduni wa mpangilio wa kijamii (mila na desturi) na utamaduni wa kiisimu. Wataalamu hawa wanaeleza lugha kama kipengele mojawapo kinachobainisha utamaduni wa watu. Hii ina maana kuwa tamaduni za dunia zinatofautiana jinsi ambavyo lugha za dunia zinavyotofautiana. Kwa hivyo, utamaduni na lugha ni mambo mawili ambayo yana uhusiano wa karibu. Lugha ni sehemu ya utamaduni wa watu wanaoitumia kama lugha yao ya kwanza. Msamiati wa lugha wakati mwingine hubeba maana za kitamaduni na vile vile hudhihirisha sifa za kitamaduni.

Kimsingi, tafsiri ni mchakato wa kiwamawasiliano ambao unahusisha uhamishaji wa taarifa kutoka lugha moja hadi nyingine. Nida na Taber (1982) wanaeleleza kwamba tafsiri inahusu kuzalisha makala katika lugha pokezi kwa kutumia visawe vya karibu sana na vya makala asilia katika viwango vya maana na mtindo. Naye Munday (2001) anafafanua tafsiri kama matokeo ya mchakato wa lugha ambapo huwezesha makala ya lugha asilia kuhamishwa hadi makala ya lugha pokezi. Tafsiri nzuri lazima iwasilishe maana asilia (Nida, 1975). Mchakato wa tafsiri huhusisha zaidi ya maana za visawe vya kiisimu kwani mtafsiri anatakiwa kufahamu athari za nje ya lugha kama muktadha wa kitamaduni.

Msimamo huo wa Nida unasisitizwa na Jakobson (Munday, 2001) anaposema kuwa kutafsiri sio tu kubadilisha ishara za lugha moja kwa ishara za lugha tofauti bali ni mchakato wa kuhamisha taarifa au ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine. Naye Catford (1965) anaeleza kuwa hakuna usawe wa kimaana katika tafsiri bali kuna usawe wa kiishara. Anaendelea kufafanua kuwa kutokana na tofauti

za lugha, usawe wa kiwango fulani tu ndio unaweza kufikiwa katika tafsiri. Kiwango hiki hubainika sio tu kupitia maana za maneno na sifa za kisarufi bali pia katika tofauti za kitamaduni.

**Uhusiano kati ya Utamaduni na Tafsiri**

Uwepo wa lugha nyingi zinazowakilisha tamaduni tofauti na umuhimu wa mawasiliano hufanya tafsiri kuwa shughuli muhimu. Mawasiliano kwa njia hii hufanikisha ubadilishanaji wa utamaduni na maarifa. Lugha haiwezi kutenganishwa na utamaduni na ni muhimu kuzingatiwa katika mchakato wa kutafsiri. Kwa upande wake, tafsiri ina dhima muhimu katika utandawazi wa utamaduni, hususan utamaduni wa mziki. Tafsiri imefanikisha mwingiliano baina ya mienendo, mila, desturi, maadili na itikadi za kidini kati ya jamii tofauti tofauti.

Wataalamu wengi wameihusisha dhana ya tafsiri na utamaduni . Kwa mujibu wa Munday (2001) mitazamo ya nadharia za awali hadi 1960 iliegemea isimu lakini kuanzia miaka ya 1970 wataalamu walianza kuzungumzia nafasi ya utamaduni katika tafsiri ambapo masuala ya kijamii, kitamaduni na kihistoria yanachukuliwa kuwa muhimu katika tafsiri. Hii ni kwa sababu tafsiri ni mchakato unaofanywa kati ya lugha na kati ya tamaduni. Inamaanisha kuwa tofauti kati ya lugha na utamaduni unaohusika huathiri mchakato wa tafsiri. Kuna muumano dhabiti kati ya lugha na utamaduni wa watu wanaotumia lugha hiyo kama lugha ya kwanza. Uhusiano huu hubainika waziwazi hasa kupitia viambajengo, dhana na maneno ya kitamaduni. Hali hii hutatiza watafsiri na hata wakalimani wanapojaribu kufasiri kwa kuzingatia uaminifu kwa makala asilia (Al-Zahran, 2003). Kutokana na hali hii tafsiri sio tu mchakato unaoziba pengo linaloletwa na tofauti za lugha bali kwa kiwango kikubwa huwa kama daraja kati ya tamaduni tofauti. Namy (1978:25) anaeleza:

> Ufasiri ... sio tu kubadilisha maneno kutoka lugha moja hadi nyingine. Ni hasa kuweka daraja la kisemantiki kati ya tamaduni mbili, mionoulimwengu miwili tofauti.

Maoni hayo ya Namy yamesisitizwa na Chama cha Wakalimani cha AIIC (*International Association of Conference Interpreters*). Katika chapisho lao la 2002a wanasema kwamba jukumu la mfasiri wa mikutano linachukuliwa kama daraja kati ya tamaduni tofauti. Kwa sababu hii tafsiri na ukalimani huchukuliwa kama mawasiliano yanayohusisha tamaduni.

Halikadhalika, Altman (1990) anasisitiza kwamba jukumu la mkalimani ni kuwezesha mawasiliano kati ya watu pasipo na vizingiti vya lugha na utamaduni. Naye Nida (1964) anashikilia kwamba lugha haiwezi kueleweka nje ya mfumo wa utamaduni ambao lugha yenyewe ni sehemu muhimu. Kwake, mtafsiri hajishughulishi tu na maneno bali pia na muktadha ambamo maneno hayo yanatumika na usawe wowote unafaa kuzingatia miktadha yote miwili, ya makala asilia na makala pokezi. Nida anahoji kwamba uelewa wa makala uegemezwe kwenye muktadha mahsusi na utamaduni wa makala asilia na pokezi. Bila hili, tafsiri haiwezi kufanikiwa. Naye Catford (1965) anakubaliana na Nida anaposema kuwa hali ya makala kutotafsirika hutokana na ukosefu wa mkutadha unaolingana na kufanana kati ya makala asilia na lugha pokezi.

Katan (2004) anaona mtafsiri kama mpatanishi wa kitamaduni ambaye anawezesha mawasiliano, maelewano na matendo kati ya watu au makundi ambayo yametengana kwa sababu ya lugha au utamaduni. Kwa sababu hii anamuona mtafsiri akitekeleza jukumu sio tu la kutoa maelezo au ufafanuzi ulio ndani ya makala bali pia kuhamisha nia, maoni, maono, hisia na matarajio ya makala asilia hadi lugha pokezi. Hii ina maana kuwa mtafsiri wa kitamaduni anafaa kuenda zaidi ya yale maelezo yaliyotolewa katika makala asilia na kuweza kujaribu kubaini yale ambayo hayakuelezwa waziwazi lakini yanaweza kukisiwa. Mtafsiri basi anafaa afahamu tamaduni husika. Kutokana na tofauti za kitamaduni kati ya lugha, zinazosababishwa na tofauti za kihistoria, kijiografia, mila na desturi na itikadi za kidini, kuna vikwazo vinavyomtatiza mtafsiri katika mchakato wa tafsiri. Naye Nord (2001) anashikilia kuwa 'kutafsiri ni kulinganisha tamaduni'. Kwa hivyo, tafsiri haihusu tu uelewa au ujuzi wa kiisimu pekee bali uelewa wa utamaduni asilia na pokezi. Tafsiri si tu uhawilishaji wa maana, bali pia uhawilishaji kati ya tamaduni. Uhalisia huu huwatatiza watafsiri.

Guo (2012) anaeleza kuwa tofauti za kitamaduni za kihistoria ni mojawapo ya matatizo yanayomkumba mtafsiri. Utamaduni wa kihistoria unahusu mila, desturi, mielekeo, amali na itikadi ya jamii fulani na ambayo jamii hiyo huja kupata katika harakati ya maendeleo ya kihistoria. Maendeleo na mabadiliko ya kihistoria ni mengi na basi utamaduni na kihistoria ni wa aina

mbalimbali. Guo anasema kuwa tofauti za miktadha ya kitamaduni ya kihistoria husababisha matatizo ya mawasiliano kati ya mataifa na jamii mbalimbali. Maoni yake ni kwamba visawe vya kipragmatiki vinafaa zaidi kwa hali kama hii kwani visawe hivi huelekeza mtafsiri kutozingatia lugha na kufanya uteuzi mradi tu makala inayotafsiriwa iweze kueleweka vizuri kwa walengwa.

Hali kadhalika, Guo (2012) anasema kwamba tofauti za utamaduni wa kiasilia hutatiza mtafsiri. Utamaduni wa kiasili unatokana na eneo la kijiografia, mazingira ya kiasili na mila za kijamii. Mambo haya huchangia kuunda utamaduni wa kiasili wa jamii fulani. Guo anataja kuwa kutokana na tofauti hizi maneno ya lugha fulani yanaweza kuwa na maana tofauti katika utamaduni tofauti. Kwa mfano, dhana ya ng'ombe katika Kiswahili ina maana husishi tofauti na jamii ya Wahindi, na dhana ya 'mbwa' ina maana husishi tofauti katika jamii za Kiafrika na jamii ya Kichina.

**Mikakati ya Kutafsiri Matini za Kitamaduni**

Wataalamu mbalimbali wamezua mbinu za kutafsiri makala kwa jumla. Mwansoko (2013) amebainisha mbinu nne: tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi, tafsiri ya kisemantiki (wazi) na tafsiri ya mawasiliano (huru). Anataja kuwa kati ya hizi, tafsiri ya kisemantiki na kimawasiliano ndizo hutumika zaidi. Hata hivyo, wataalamu kama Nida na Guo wamejaribu kutatua tatizo linalosababisha ugumu wa kutafsiri matini kwa sababu ya tofauti za kitamaduni. Wanapendekeza mbinu za usawe wa kisemantiki na kipragmatiki, uasilishaji na ugenishaji, usawe wa kiumbo (usahilishaji) na usawe wa kiuamilifu.

**Mbinu za Usawe wa Kisemantiki na Kipragmatiki**

Kwa maoni ya Guo (2012) suluhu la tatizo la kutotafsirika kwa matini ya kitamaduni ni kutafuta visawe vya kitamaduni. Anaendelea kusema kuwa usawe wa kitamaduni ni wa aina mbili: usawe wa kisemantiki na usawe wa kipragmatiki. Maana kisemantiki humwongoza mtafsiri kutafuta tafsiri maana ya neno kwa njia mbili: maana rejeshi ya neno na maana husishi ya neno. Maana rejeshi ya neno hueleza na kufafanua maneno yote ambayo yanaweza kurejelewa na neno fulani. Nayo maana husishi ya neno ni maana inayatokana na muktadha (wa kitamaduni au wa kiisimu) ambamo neno fulani hutokea mara kwa mara. Maana husishi ya neno hurejelea maana ya kitamaduni kwani huzingatia muktadha maalum. Mtafsiri anaweza kutumia mkakati huu katika kutafuta visawe anapotafsiri matini za kitamaduni.

Usawe wa kipragmatiki huzalisha visawe vyenye maana inayotokana na muktadha. Muktadha huu unahusu tajiriba ya mzungumzaji na msikilizaji, na muktadha wa kiisimu na sifa nyingine nje ya sifa za kiisimu kama toni na ishara, utamaduni na mtindo au sajili. Makala hii haikuchunguza iwapo tafsiri za Kiswahili katika uwanja wa bunge na serikali zimezingatia muktadha wa kijamii utamaduni wa kihistoria, na kijamii. Usawe wa kipragmatiki hauhusishi sana maana ya neno au sentensi bali husisitiza uwezekano wa kupata maneno ambayo msomaji pokezi ataweza kuyaelewa vizuri katika muktadha fulani.

**Mbinu za Uasilishaji na Ugenishaji**

Mbinu nyingine ambazo zinaweza kutumiwa katika kutafsiri matini za kitamaduni ni uasilishaji na ugenishaji. Hii ni mikakati ya kimsingi ambayo inaweza kumsaidia mtafsiri. Uasilishaji ni aina ya tafsiri ambapo mtafsiri huamua kutumia tafsiri wazi yenye mtindo sahili ili kuondoa ugeni wa makala au dhana za kigeni kwa hadhira ya lugha lengwa. Ugenishaji hutokea ambapo mtafsiri huamua kuvunja kaida za lugha pokezi na kuhifadhi ugeni katika makala tafsiriwa.

Eugene Nida ni kielelezo cha wataalamu ambao wanapendekeza uasilishaji huku Lawrence Venuti akipendekeza ugenishaji katika tafsiri. Kwa mujibu wa Venuti (1995) uasilishaji hurudisha chini thamana ya makala ya kigeni ili ifikiane na amali za kitamaduni za lugha pokezi. Kwa upande mwingine anasema kuwa ugenishaji hulazimisha amali za utamaduni mpya na kudhihirisha tofauti za kitamaduni za makala yenye utamaduni wa kigeni na kuwezesha msomaji kusafiri nje ya utamaduni wake.

Uasilishaji basi ni aina ya tafsiri iliyo wazi na iliyowasilishwa kwa mtindo wa moja kwa moja ili kuondoa ugeni wa makala yenye utamaduni wa kigeni. Ugenishaji ni pale ambapo makala ya kigeni hutafsiriwa kwa kuvunja kimaksudi kaida za lugha pokezi kwa kuhifadhi ugeni wa makala asilia

(Shuttleworth & Cowie, 2014). Kimsingi, katika kutafsiri makala ya kitamaduni, kwa kutumia mbinu ya uasilishaji mtafsiri hubadilisha utamaduni wa makala asilia na kuweka utamaduni pokezi. Dhana za utamaduni asilia hubadilishwa na za utamaduni pokezi. Vile vile, katika mbinu ya ugenishaji mtafsiri huhifadhi tofauti kati ya tamaduni zote mbili. Mbinu hizi hutumiwa pale ambapo kuna tofauti katika uwasilishaji kiisimu na katika maana husishi kitamaduni.

**Mbinu za Usawe wa Umbo na Usawe Amilifu**

Nida (2001) anasema kuwa ili tafsiri iwe fanikivu lazima izingatie tamaduni mbili zinazohusika kuliko kuzingatia tu lugha mbili zinazohusika. Maoni yake ni kwamba maneno ya lugha hupata maana katika muktadha wa utamaduni unaohusika. Anaona tofauti za kitamaduni kama kikwazo kikubwa katika mchakato wa kutafsiri. Nida anabainisha aina mbili za usawe katika tafsiri: Usawe wa umbo na usawe amilifu.

Tafsiri ya usawe wa umbo hulenga zaidi ujumbe na umbo la makala asilia. Ni maelezo yanayozingatia kwa dhati msamiati, sarufi na umbo la makala na kuhamisha hadi lugha pokezi. Hii ni tafsiri sisisi. Tafsiri ya usawe amilifu inalenga hasa athari ya makala asilia na kuhakikisha kuwa msomaji wa makala tafsiriwa anapata athari sawa na ya msomaji wa makala asilia. Nida anasisitiza kwamba msomaji wa makala pokezi anafaa kuyaelewa makala tafsiriwa kwa kiwango cha kuyafahamu jinsi wasomaji asilia huenda walifahamu na kuathiriwa na makala hayo. Kwa maneno yake, Nida (1995:118) anasisitiza kuwa 'msomaji pokezi aweze kufahamu na kupata athari sawa na ya msomaji asilia'. Kwa sababu ya mtafsiri kutia juhudi ili kuweka ujumbe wazi kwa walengwa, Nida anapendekeza tafsiri hii kwani kwake inaondoa kutoeleweka kwa matini kwa hadhira na inarejelea hali ya sasa.

Mfumo wa serikali unaoendeshwa katika nchi za Kiafrika ni wa kigeni. Bara la Afrika liligawanywa na mataifa ya Kimagharibi kule Berlin mnamo mwaka wa 1884. Kabla ya hapo, bara la Afrika lilijumuisha jamii mbalimbali ambazo zilikuwa na mifumo tofauti tofauti ya uongozi na kila jamii iliendesha shughuli zake kwa kuzingatia miundo yao ya kiasili. Hata hivyo, baada ya kongamano la Berlin, bara la Afrika liligawanywa katika maeneo bainifu. Dhana ya nchi kwa misingi ya Kimagharibi ilizaliwa wakati huo. Kwa sababu hii, dhana zinazohusu mfumo wa serikali na utawala ni ngeni na nyingi hazikuwa na visawe katika lugha nyingi za Kiafrika, Kiswahili kikiwemo. Utamaduni wa historia ya bara la Afrika unabainika kupitia uwanja wa serikali na bunge kwani asasi hizi zinachota kutoka utamaduni wa Kimagharibi.

Makala hii inachunguza baadhi ya dhana za serikali na bunge kwa kutoa mifano ya bunge la Afrika na kubainisha mbinu zilizotumiwa katika kutafsiri dhana hizo. Vile vile, makala inatathmini iwapo mbinu hizo zinawasilisha ujumbe na kudhihirisha mbinu ambayo imetumiwa kwa wingi katika tafsiri hizi. Data ya makala hii ilitokana na vyombo vya habari na vikao vya bunge la Afrika. Msamiati wa shughuli za bunge na serikali pamoja na tafsiri zake umechunguzwa na kubainisha mbinu zilizotumiwa katika kutafsiri kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Mbinu ambazo zimetumiwa ni usawe amilifu, usawe wa kipragmatiki, usawe wa kisemantiki, uasilishaji na ugenishaji. Data yenyewe imewasilishwa hapa chini.

**Jeswali la 1: Msamiati wa Serikali unaotumiwa katika Bungela Afrika**

| | **Kiingereza** | **Kiswahili** | **Mbinu** |
|---|---|---|---|
| 1. | *Democracy* | Demokrasia | Ugenishaji |
| 2. | *Summmit of Head of State and Government* | Mkutano wa wakuu wa nchi na serikali | Usawe amilifu/usawe wa umbo |
| 3. | *Change of Government* | Kubadilisha serikali | Usawe wa kisemantiki |
| 4. | *Government Officials* | Maafisa wa Serikali | Usawe wa kisemantiki |
| 5. | *Monarchy* | Tawala za kifalme | Usawe wa kipragmatiki |
| 6. | *Candidate* | Mgombea kiti | Ugenishaji |
| 7. | *Ballot paper* | Karatasi ya Kupiga kura | Usawe wa umbo/amilifu |
| 8. | *Separation of Power* | Kutenganisha majukumu | Usawe wa umbo/amilifu |
| 9. | Executive Council | Baraza la Mawaziri | Uasilishaji |
| 10. | *Ghost of Poverty* | Jinamizi la Umaskini | Usawe wa umbo/amilifu |
| 11. | *Weapons of mass destruction* | Silaha za maangamizi | Usawe wa umbo/amilifu |
| 12. | *Expenditure* | Matumizi ya fedha | Usawe wa umbo/amilifu |
| 13. | *Overdraft* | Kukopa | Usawe wa umbo/amilifu |
| 14. | *Operational Budget* | Bajeti ya kazi za kila siku | Usawe wa umbo/amilifu |
| 15. | *Broadening partnership* | Kupanua ushirikiano | Usawe wa umbo/amilifu |
| 16. | *Annual Budget* | Bajeti ya Mwaka | Ugenishaji |
| 17. | *Open Tender* | Kufungua Tenda | Ugenishaji |
| 18. | *Development Partners* | Wadau katika maendeleo | Usawe wa Kisemantiki |
| 19. | *Member States* | Nchi wanachama | Usawe wa umbo/amilifu |
| 20. | *Senate* | Seneti | Ugenishaji |
| 21. | *County* | Kaunti | Ugenishaji |

Jedwali la 1 linabainisha sampuli ndogo ya msamiati wa serikali unaotumika katika Bunge la Afrika. Kama ilivyotajawa hapo juu, ni msamiati wa kigeni kutokana na tofauti za utamaduni wa kihistoria kati ya nchi za kimagharibi na za Kiafrika. Asili mia kubwa ya msamiati huo umetafsiriwa kwa Kiswahili kwa kutumia mbinu ya usawe amilifu. Mbinu hii inatafsiri dhana kwa kuhakikisha kuwa ujumbe unawafikia na kuwaathiri kwa namna inavyowaathiri wasomaji asilia. Vile vile, tafsiri hizi zimesahilishwa kwa kutumia lugha rahisi inayoeleweka kwa hadhira ya sasa. Kwa njia hii basi mifano hiyo pia inazingatia usawe wa umbo. Tafsiri hizi zinaonekana kulenga zaidi ujumbe asilia na kutokea kama maelezo ambayo yanalenga kuhamisha maana katika lugha asilia hadi pokezi kwa njia ya moja kwa moja. Tafsiri hizi zinaonyesha jitihada za watafsiri kuweka ujumbe wazi kwa walengwa jinsi ambavyo Nida anavyopendekeza.

Kwa mfano, neno 'ballot paper' limetafsiriwa kuwa 'karatasi ya kupiga kura' 'weapon of mass destruction' limetafsiriwa kuwa 'silaha za maangamizi'. Tafsiri za Kiswahili ni sahili na zinaeleweka kwa urahisi. Vile vile, dhana ya 'operational budget' inatafsiriwa kama 'bajeti ya kazi za kila siku' nayo 'overdraft' inatafsiriwa kuwa 'kukopa'. Tafsiri hizi zote ni nyepesi na rahisi kueleweka kwa mtafsiri.

Mbinu ya ugenishaji imetumiwa hasa pale ambapo dhana ya Kiingereza haina kisawe chake katika Kiswahili na pengine maelezo yatakuwa marefu. Kwa mfano, dhana ya 'democracy' inatoholewa na kuwa 'demokrasia' ambapo inahifadhi ugeni wake katika Kiswahili. Mifano mingine ni '*Senate*', '*County*', '*annual budget*', '*open tender*' na '*candidate*'. Ingawa dhana hizi zinahifadhi ugeni katika Kiswahili zinarutubisha msamiati wa Kiswahili kwa kulazimika kukopa dhana mpya.

Mbinu ya usawe wa kipragmatiki imetumika kupitia neno '*monarchy*' ambalo limetafsiriwa kama 'tawala za kifalme'. Mbinu hii huzingatia maana ya neno kwa kuangalia muktadha wa mpokezi. Muktadha huu huhusisha pia tajriba za mpokezi. Kwa vile jamii za Kiafrika zilikuwa na mfumo wa kifalme katika uongozi wa kiasili, dhana hii inaeleweka vizuri kwa mpokezi. Pia dhana ya 'executive council' imewasilishwa kama 'baraza la mawaziri'. Katika jamii za Kiafrika kulikuwa na mfumo wa baraza la wazee ambao walitoa mwelekeo kuhusu mambo mbalimbali ya kijamii. Kwa sababu hii, dhana ya 'baraza la mawaziri' inatoa taswira nzuri ya dhana ya Kiingereza. Mbinu hii hujaribu kuchukua dhana za kigeni na kuziwasilisha katika mazingira pokezi kwa kuzipa uasili wa namna fulani. Ugeni wa dhana hizo umeondolewa kiasi cha 'kuziasilisha' kwa msomaji pokezi. Mbinu hii husaidia kufanya makala kueleweka kwa wasomaji lengwa.

Tafsiri zilizowasilishwa hapo juu na ambazo zinatumiwa zinaeleweka vizuri. Ni wazi kuwa msamiati wa serikali unaweza kutafsirika vizuri kwa kutumia mbinu za usawe amilifu, usawe wa umbo, usawe wa kipragatiki, uasilishaji, ugenishaji na usawe wa kisemantiki. Jedwali la 2 linabainisha sampuli ndogo ya msamiati wa bunge na tafsiri zake. Msamiati wa bunge ni wa utamaduni wa Kimagharibi. Hata hivyo, mbinu zilizotumiwa zinawasilisha maana asilia kwa usahihi. Dhana ya kigeni '*August House*' imetafsiriwa kwa Kiswahili kuwa 'bunge' Mbinu ya uasilishaji imetumiwa kwani neno 'bunge' limekopwa kutoka kwa lugha ya Kisukuma. Mbinu ya usawe wa kipragmatiki ndiyo imetumiwa sana kuwasilisha dhana za '*commencement of business*', '*communication from chair*', '*ordinary sessions*', '*rules of procedure*', '*point of order*', '*point of correction*', na '*point of procedure*'. Mbinu hii inalenga kuzalisha maana inayotokana na muktadha. Katika mifano hiyo muktadha wa bunge unaongoza mtafsiri kufasiri maana na kuiwasilisha katika lugha pokezi. Maana inayowasilishwa inaeleweka katika muktadha wa bunge. Kwa mfano, '*commencement of business*' inaweza kuwa na maana tofauti katika muktadha tofauti.

**Jedwali la 2: Msamiati wa Bunge unaotumika katika Bunge la Afrika**

| | Kiingereza | Kiswahili | Mbinu |
|---|---|---|---|
| 1. | *August House* | Bunge | Uasilishaji |
| 2. | *Order Paper* | Orodha ya Shughuli | Usawe amilifu/usawe wa umbo |
| 3. | *Presentation and Debate* | Kuwasilisha na kujadili | Usawe amilifu/usawe wa umbo |
| 4. | *Adjournment of House* | Kuahirisha bunge | Uasilishaji |
| 5. | *Assembly Approval* | Uidhinishaji wa bunge | Uasilishaji |
| 6. | *Commencement of business* | Kuanza kwa shughuli | Usawe wa kipragmatiki |
| 7. | *Communication from chair* | Taarifa ya Spika | Usawe wa kipragmatiki |
| 8. | *Ordinary Sessions* | Vikao vya Kawaida | Usawe wa umbo/usawe amilifu |
| 9. | *Rules of Procedure* | Kanuni za bunge | Usawe wa umbo/usawe amilifu |
| 10. | *Clerk of Parliament* | Karani wa bunge | Usawe wa umbo/umbo amilifu |
| 11. | *Plenary* | Kikao cha Pamoja | Usawe wa umbo/usawe amilifu |
| 12. | *Legislative Organ* | Chombo chenye mamlaka ya kutunga sheria | Usawe wa umbo/ usawe amilifu |
| 13. | *Point of order* | Hoja ya utaratibu | Usawe wa kipragmatiki |
| 14. | *Point of Correction* | Hoja ya Urekebishaji | Usawe wa kipragmatiki |
| 15. | *Point of Procudure* | Hoja ya Mwongozo | Usawe wa kipragmatiki |
| 16. | *Bureau* | Mikutano ya Uongozi wa Bunge | Usawe wa umbo/usawe amilifu |

Mbinu za usawe wa umbo na usawe amilifu pia zimetumiwa. Usawe wa umbo huzingatia lugha sahili inayoweza kueleweka kwa hadhira, ilhali visawe amilifu hulenga kutoa athari sawa na ya msomaji wa makala asilia. Dhana ya '*legislative organ*' imetafsiriwa kuwa 'chombo chenye mamlaka ya kutunga sheria'. Tafsiri hii ni sahili na ya kueleweka kwa urahisi. Mbinu ya ugenishaji haikutumiwa katika mifano tuliyotoa. Kwa jumla, tafsiri zilizotolewa ni mwafaka na zinaafiki ujumbe uliopo kwenye lugha asilia.

**Hitimisho**

Kutokana na uchanganuzi wa msamiati wa serikali na bunge unaotumiwa katika Bunge la Afrika, imebainika kuwa mbinu mbalimbali zimetumiwa katika kuutafsiri. Mbinu zilizotumiwa ni: usawe wa umbo, usawe amilifu, usawe wa kipragmatiki, usawe wa kisemantiki, ugenishaji na uasilishaji. Mbinu ya uasilishaji inapotumiwa neno la kigeni huchukua dhana katika mazingira ya Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika. Kwa mfano, 'bunge' na 'baraza'. Baadhi ya maneno yanahifadhi ugeni katika lugha na utamaduni wa Kiswahili. Maneno kama haya yanakopwa na kutoholewa kwa mfano, '*democracy*', '*budget*', '*senate*', '*county*' na '*tender*'. Baadhi ya msamiati wa Kiingereza ulitolewa maelezo sahihi kwa ajili ya hadhira kupata maana ya dhana bila tatizo hasa kwa kuzingatia miktadha ya maneno hayo. Kwa mfano, '*order paper*' na '*communication from chair*' yalitafsiriwa kama 'orodha ya shughuli' na 'taarifa ya spika' mtawalia. Tafsiri hizi ni sahili na zinaeleweka katika mazingira ya bunge. Kutokana na uchanganuzi huu, imebainika kuwa mbinu zilizojadiliwa zinaweza kutumiwa kutafsiri matini za utamaduni.

**Marejeleo**

AIIC (2002). Media Interpreting – A Different Sort of World (online) Geneva: AIIC available at http://www.aiic.net/view page.cfm/page 149.

Altman (1990). What helps effective communication? Some interpreters' views. *The Interpreters Newsletter 3*. Kur. 23 – 32.

Al-Zahran, A. (2003). Translators and Culture – Specific References: A Relevance Theoretic Approach to Arabic-English – Arabic Translation. University of Salford: Unpublished M.A. Thesis.

Bryam, M. (2008*). From Foreign Language Education to Education for Intercultural Citizenship: Essays or Reflections.* Clevedon: Multilingual Matters.

Catford,J.C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation. Oxford:* Oxford University Press.

Guo, H. (2012). A Brief Analysis of Culture and Translation *Theory and Practice in Language Studies* Vol. 2, No. 2. Kur. 343 – 347.

Katan, D. (2004). *Translating Cultures: An Introduction for Translators, Interpreters and Mediators.* London & New York: Routldege.

Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications.* New York: Routledge.

Mwansoko, H.J.M. (2013). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu.* Dar es Salaam: TUKI

Namy, C. (1978). Reflections on the Training of Simultaneous Interpreters: A Metalinguistic Approach. Katika Gerver, D. na Sinaiko, H.W. (wah,) Kur. 25 – 33.

Nid,E. A. (1975). *Language Structure and Translation,* Stanford: Stanford University Press.

Nida, E.A. (1964). *Towards a Science of Translation.* Leiden: E.J. Brill

Nida, E.A. (2001). *Contexts in Translation.* Amsterdam/Philadelphia:John Benjamins .

Nida, E.A. na Taber C.R. (1982). *The Theory and Practice of Translation.* Leiden, E. J. Brill.

Nord, C. (2001). *Translating as a Purposeful Activity – Functional Approaches Explained,* Shangai:Shangai Foreign Language Education Press.

Shuttleworth, M. & Cowie M. (2014): *Dictionary of Translation Studies.* New York:Routledge.

Venuti, L. (1995). *The Translater's Inability: A History of Translation,* London: Routledge.

Venuti, L. (1998). *The Scandles of Translation :Towards an Ethics of Difference.* London: Routledge.